**Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**Kukithiri kwa Mauaji ya Kutisha ya Wanawake yanayotokana na mahusiano ya wanandoa, wapenzi ama watoto wao.**

Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa chini ya sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002. Mtandao huu unaoundwa na takribani wanawake 60 watetezi wa haki za binadamu wenye dira ya kuona kuwa katika Wanawake na wasichana wa Tanzania wanaishi maisha ya furaha na kufurahia utu wao bila ya kuwa bughudha, udhalilishwaji wala ukatili wa Kijinsia.

Nchi yetu ni miongoni mwa nchi imeridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya kulinda utu wa Mtu na kulinda haki ya kuishi; Mfano wa baadhi ya Mikataba hiyo ni pamoja na a) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu(1948), b) Mkataba wa Kuondoa aina zote za ukatili wa kijinsia kwa Wanawake (1979) na mingine mingi ya kulinda haki za wanawake na wasichana dhidi ya uonevu.

Serikali yetu ya Jamuhuri wa Muungano wa Tannzania imeenda mbali zaidi kwa kuyachukua maadhimio ya tamko la kimataifa la Haki za binadamu (1945) na kuyaweka maadhimio haya kwenye Katiba Ya Jamhuiri ya Muungno wa Tanzania ya Mwaka 1977. Sheria ya Makosa ya Adhabu Sura ya 16, na sera za nchi nyingi zinazotoa kipaumbele cha ulinzi na usalama kwa wanawake na wasichana pamoja na makundi mengine dhidi ya ukatili wa kijinsia. Tunaishukuru serikali yetu kuweka madawati ya jinsia kwenye idara mbali mbali za serikali ili kufanyia kazi masula ya ukatili wa kijinsia yanapofika katika vituo vya polisi ama idara za taasisi za kiserikali ndani ya wizara. Tunaishukuru pia serikali yetu kuwa na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kupunguza ukatili dhidi ya Wanawake na watoto (MTAKUWWA) ambao unaisha mwaka huu wa mwaka 2022.

Pamoja na hayo yote, suala la mauaji ya Wanawake kuuliwa na wenza wao au watoto wao wa kuwazaa linaongezeka na kuchukua sura tofauti tofauti. Japo hakuna takwimu kamili, lakini taarifa za vyombo vya habari na matukio yanayooneshwa na kutolewa taarifa kila siku ama kila wiki yanaonesha kuwa mauaji haya ni mengi na yanazidi kushika kasi sana. Mf. 1)Tukio la Mwanamke Mfanyakazi ya Banki ya CRDB Mwanza kuuwawa na mwenza wake na kukamatwa akiwa na mwili wa marehemu mkewe kwenye gari akielekea kuutupa, 2)Msichana wa chuo Kikuu cha Kilimo SUA aliyeuawa na Mpenzi wake na mwili wake kwenda kuzikwa nyumbani kwao Kilimanjaro, 3) Mwanamke kukatwa masikio mawili huko Rukwa (Sumbawanga) hii ilikuwa ni nusu kifo. 4) Mtoto kumuuwa mamake huko Mererani Arusha 5) Mtoto kumuuwa mama yake Kilimanjaro, 6) Mfanyakazi wa Milembe Hosipitali Rufina Komba kuuwawa kwa kukatwa katwa mapanga na kuchomwa moto na mumewe huko Dodoma (8.1.2022), 7) Msichana Betila Lucas wa Miaka 17 kuuwawa na mumewe Dodoma ( 9.1.2022). 8) Jana Jioni ya tarehe 12.1.2022 Tumepokea pia simu kutoka kwa Wanachama wenzetu kuwa kuna mwanamke huko Butiama amekatwakatwa sehemu zake za siri na mumwewe kisa ni wivu wa mapenzi.

Ikumbukwe kuwa utitiri wa matukio haya umetokea kipindi kifupi mfululizo na matukio haya yanafanywa na ndugu wa karibu, mume, mtoto au mpenzi anayeaminiwa kwa kisingizio cha wivu ama tamaa ya mali.

**Tunatoa rai kwa;**

1. Vyombo vyote vya serikali ikiwemo Mh.Rais na Viongozi wote kutekeleza kwa vitendo Katiba na Sera na viapo vyao walivyoahidi kulinda watu na mali zao kwa kutoa ulinzi kamili kwa wanawake wote dhidi ya vitisho na mauaji. Kwa sasa Matukio haya yanaichafua nchi kwa kuashiria tunanyemelewa na uvunjifu wa amani.
2. Kamati za Ulinzi wa wanawake na watoto zifanye kazi kikamilifu kuibua migogoro ambayo ni tishio kwa maisha ya wanawake na watoto na kutoa taarifa kwa wahusika kuzuia madhira haya kwani ukatili huu hautokei siku moja tu, huanza taratibu na kuwa sugu.
3. Viongozi wa kiroho kusaidia kuelimisha waumini wao na kuwa msaada penye viashiria vya kifo na kuepuka misimamo hatarishi inayoweza kuwaletea hatari ya kifo waumini wao.
4. Wazazi na jamii kusaidia watoto wao wa kike wanapoleta mashauri hatarishi kwa maisha ya binti zao badala ya kusimamia au kutaka ama kuficha ukweli au

kufurahisha jamii kwa kuwahimiza wavumilie mahusiano hatarishi kwa uhai wao.

5. Maofisa ustawi wa jamii wachukue jukumu la kuisimamia jamii kutatua matatizo katika jamii. wasaidie kutoa ushauri sahihi na kupeleka mashauri kwa wataalamu wa afya ya akili au vyombo vingine vya dola kwa msaada zaidi.
6. Eneo la afya ya akililiangaliwe upya kwa kuona jamii inapataje elimu ya kupunguza misongo ya mawazo kwa mtu mmoja mmoja na kuwa na uwezo wa kukabili msongo wa mawazo na si kuzihamisha kwa mwingine na kusababisha majeraha au vifo.
7. Madawati ya jinsia yaongeze uchunguzi na njia zaidi za kupambana kuzuia ukatili usifikie hatua za mauaji.
8. Kila familia ione ina wajibu kuchangia katika ulinzi wa watoto wao wa kike kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwani ni watu wa kwanza kujua hali tetekatika mahusianoya nduguzao hivyo kuwaokoa kwa wakati kutoka katika kifo.
9. Ifikie mahali wanajamii nao wachukue hatua za kuwalinda wanawake badala ya dhana ya kutoingilia mahusiano ya wenzi hivyo ata wanapoombwa msaada kwenye hatari wajitokeze klwa wingi kusaidia.
10. Wakati umefika wa kuwa na sheria inayokataza ukatili wa kijinsiainayojisimamia ili kukabiliana na changamoto zinazokithiri
11. Vyombo vya habari view chachu ya kuelimisha na kuibua matukio haya na kuichagiza serikali na wadau kuchukua hatua.
12. Sisi watetezi wa haki za binadamu pamoja na wanaharakati tuanzishe program kwa kushirikiana na serikali zitakazo kwenda moja kwa moja katika jamii ili kutatua changamoto za kijamii.
13. Watuhumiwa kuchukuliwa hatua stahiki, za kisheria kwa wakati, kwani tumeona kutokuchukuliwa hatua za haraka kwa watuhumiwa wa vitendo vya ukatili Mfano Mtuhumiwa wa aliyemkata masikio mwenza wake katika matukio aliyokuwa akiyafanya kwa wenza wake waliopita hivyo kupelekea vitendo hivyo kuendelea kwa kukithiri.

**Imetolewa na:**
**Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za binadamu Tanzania**
**Leo Tarehe 13.1.2022.**